

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA SABA

21 SEPTEMBER, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA SABA – TAREHE 21 SEPTEMBER, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

95. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-


Je, kuna mkakati gani wa kuwarasimisha Vijana waliopata ujuzi nje ya mfumo rasmi.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

96. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza mkakati wa ujenzi wa Hosteli kwenye Shule za Kata.



97. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Mradi wa Dar es Salaam *Metropolitan Development Project* Awamu ya Pili utaanza katika Jimbo la Kigamboni.

**98. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON
MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itafanya maboresho ya ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya vya Chikobe na Bukoli.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**99. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO
(WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini Wananchi wenye sifa wa Shehia ya Njuguni, Majenzi na Chomboni – Micheweni wataunganishwa na TASAF.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

100. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mikakati gani ya kuelimisha Wananchi wanaozunguka Hifadhi za Misitū biashara ya uuzaji/utunzaji wa Hewa ya Ukaa.

WIZARA YA AFYA:

101. MHESHIMIWA MWANTUM DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kwa nini Ugonjwa wa TB hauwezi kuonekana kwa mara moja unapompata muathirika.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

102. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa Wananchi waliopisha maeneo ya Jeshi kama Cheju na Dunga Zanzibar.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

103. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Barabara ya Kolandoto – Mhunze hadi Mwangongo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

104. MHESHIMIWA MOSHI SELEMAN KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa ardhi kati ya Vijiji vya Vikonge na Nomalusambo dhidi ya TFS.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

105. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali italipa madai ya Shilingi Trilioni 7.91 ya watoa huduma kama yalivyoripotiwa kwenye ripoti ya CAG 2021.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**106. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON
PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Shirika la Nyumba la Taifa litaanza
Ujenzi wa Safari City nje kidogo ya Jiji la Arusha.

**107. MHESHIMIWA SOPHIA HERBON
MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Wapimaji wa Ardhi,
katika Mji wa Tukuyu Wilayani Rungwe ili
kupunguza Migogoro ya Ardhi.

WIZARA YA KILIMO:

**108. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Wataalam wa zao la Zabibu Dodoma.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

109. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, kwa miaka 10 ni Wawekezaji wangapi wa nje walionyesha nia ya kuwekeza na kufanikiwa na upi mkakati kwa ambao hawajafanikiwa.

110. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itawawezesha Wananchi wa Jimbo la Tarime Vijijini, Tarime Mjini na Rorya kupata bidhaa kutoka nchi jirani ya Kenya.

**111. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO
(NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji,
Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Mifuko ya kuwezesha Wananchi
kiuchumi itaunganishwa ili kuleta tija na manufaa
kwa Watanzania hasa waishio Vijijini.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**112. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA
(MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo
cha VETA katika Wilaya ya Manyoni.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**113. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na
Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itabadili utaratibu kuwataka Wavuvi wanaotumia *RingNet* kutoruhusiwa kuvua mchana na kuvua chini ya mita 50.

IV. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

**DODOMA
21 SEPTEMBER, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**